Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili ab initio – Standard level – Paper 1
# Swahili ab initio – Niveau moyen – Épreuve 1
# Swahili ab initio – Nivel medio – Prueba 1

Monday 8 May 2017 (afternoon)
Lundi 8 mai 2017 (après-midi)
Lunes 8 de mayo de 2017 (tarde)

1 h 30 m

---

**Text booklet – Instructions to candidates**

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

**Livret de textes – Instructions destinées aux candidats**

- N’ouvrez pas ce livret avant d’y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l’épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

**Cuaderno de textos – Instrucciones para los alumnos**

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.



2217–2835
© International Baccalaureate Organization 2017

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional


https://xtremepape.rs/

**Matini A**

**Kijana mvivu na babake mvuvi**

Mvuvi mmoja alikuwa na kijana wake mvulana. Kijana huyu alipenda chakula kimoja tu, samaki. Alikula samaki asubuhi, mchana na jioni. Kazi ya babake ilikuwa ni kuvua samaki ili kijana wake apate kula.

Ubaya ni kwamba kijana wa mvuvi alikuwa mvivu mno. Kazi kubwa aliyoweza kufanya pale nyumbani ni kula samaki. Usidhani alikula samaki wabichi. Hapana. Alichomewa kwenye moto wa kuni au makaa. Wakati mwingine alipikiwa kwa kuchemshiwa katika chungu na mara nyingine alikaangiwa kwenye kikaango. Kazi hii ya kuchoma, kuchemsha na kukaanga ilifanywa na mamake mvulana huyu.



Kila siku baba alimwambia kijana wake, “Twende tukavue samaki ili na wewe ujue jinsi ya kuvua”. Kijana alikataa katakata kwa sababu alikuwa mvivu sana. Baba alichoka kumwambia mwanawe aende naye kujifunza kuvua samaki.

Kijana mvivu aliendelea kula jasho la baba yake. Baba hakuona ubaya kumlisha mtoto wake lakini ndani ya moyo wake, alijua kwamba mtoto wake alihitaji kuwajibika.

Baada ya miaka mitano, babake akawa mgonjwa na hangeweza kuvua samaki tena kwa sababu ya unyonge. Kijana mvivu alihuzunika sana. Alipohisi njaa, alimwomba mama yake ampe samaki. Mama alimtolea vifaa vya kuvulia samaki kama vile jarife na ndoana. Alimwambia, “Mwanangu, nenda ukavue samaki ulete nikupikie”.

Kijana mvivu hakujua kuvua samaki. Alipofika baharini, aliwauliza vijana waliokuwa kando kando ya maji, “samaki wako wapi?” Walimjibu, “Wamo ndani ya maji, chini kabisa kusikoonekana kwa macho”. Kijana mvivu aliposikia hivyo alijitupa ndani ya maji akiwa na vifaa vyake mikononi. Alifikiri hiyo ndio njia ya kwenda kuwakamata samaki, lakini wapi! Alijipata katika hatari ya kuzama kwenye maji kwani alikuwa hata hajui kuogelea. Vijana wenzake walipoona kuwa anaangamia, walijirusha ndani ya maji na kupiga mbizi kuelekea upande wake na kumwokoa.

Alishikwa na aibu kwa hufanya jambo la hatari bila kupata mwelekeo. Aliwashukuru vijana wenzake kwa kumwokoa kutokana na hatari ya kuangamia majini. Alienda kumwomba msamaha babake kwa kutofuata ushauri wake na kutowajibika. Baba alifurahi kwamba kijana wake alipata mafunzo hata kama ni kwa njia ngumu. Baba alimwambia mwanawe, “ajizi ni nyumba ya njaa”.

Matini imetoholewa kutokana na Wallah Bin Wallah, *Kiswahili Mufti, Darasa la Nne* (2001)

https://xtremepape.rs/

**Matini B**

## Mahojiano baina ya Bw. Paluku Mivimba (Kiongozi wa Muungana wa wakulima) na ripota wa Wakulima Amkeni

**Ripota:** Bwana Kiongozi, tayari Muungano wa vikundi vya wakulima wa Kongo ya Kidemokrasia unafikiria jinsi ya kuwa na benki kwa faida ya wakulima. Ni kitu gani kitakachowavutia kama wakulima kutokana na benki hiyo?

**Paluku Mivimba:** Wazo hilo limetokana na kuwa ukulima au kilimo ni kazi kama zingine. Kwa hivyo sasa ukulima hauwezi kuendelea bila pesa. Ukulima unahitaji pesa za kuendesha kazi za shamba za kulima, kuvuna na kuuza mazao ya shamba. Muungano wa wakulima umeona kwamba hakuna benki zinazohudumia wakulima kikamilifu. Imeonekana kwamba zile benki za mkopo za kilimo haziendeshi vyema kazi hizo kwa faida ya huyo mkulima. Hii ni kwa sababu benki hizo zinaweza kutoa mkopo tu kwa mkulima wakati ambapo amemaliza kuvuna ama anapouza mazao yake. Basi ni kupitia huo ukosefu wa kuhudumia mkulima katika kazi zake zote ndipo Muungano wa wakulima unawafahamisha wakulima kwamba hiyo itakuwa ni benki ya ushirika na wao wenyewe watawekeza mali yao. Kila mkulima atakayetaka kuwa mwanachama atatoa mchango wa mwanachama. Akiba yake ndiyo itampa uwezo wa kuomba mkopo ili aendeshe kazi zake za kilimo. Na vile vile tukumbuke kwamba mkopo si zawadi. Ni deni! Mkulima atakapochukua mkopo kwenye benki sharti afahamu kwamba atalipa ili wakulima wengine waweze kupewa.

**Ripota:** Je, benki hiyo itasaidia mkulima kuboresha maisha yake?

**Paluku Mivimba:** Kupitia ukulima, mkulima hupata kila kitu cha kuendesha maisha yake na jamii yake. Kupitia benki hii, wanachama watapata kwa mfano pesa za kununua mbegu nzuri, mbolea na vyombo vya kazi vya shambani. Nadhani kwa kupata mkopo, maisha ya mkulima yatakuwa bora zaidi. Benki hii inaweza kugeuza maisha ya mkulima iwapo atachukulia ukulima kama biashara.

**Ripota:** Bwana Kiongozi wa Muungana wa wakulima, mkulima ni mtu gani hasa?

**Paluku Mivimba:** Mkulima ni yeyote anayeishi kwa ukulima yaani kwa yale anayotoa shambani, mifugo na upandaji. Kazi za mkulima ni nzuri. Hakuna nchi ambayo haina mkulima. Kila mmoja hawezi kwenda ofisini kwake bila kula chakula cha mkulima. Ni vyema kwa mkulima kufahamu kwamba kazi zake ndizo zinazoendesha kazi za wengine.

**Ripota:** Mwisho, Bwana Kiongozi, unawapa mawaidha gani wakulima wote?

**Paluku Mivimba:** Kwanza kabisa, nawapongeza wakulima wa mitaa ya Masisi, Rutshuru na Nyiragongo kwa bidii yao. Kisha ninawaomba wakulima wote wanaoishi huko kwao vijijini, watie bidii zaidi katika kazi zao za ukulima. Watakapofanya hivi, wataona faida kubwa ya ukulima. Asante.

Matini imetoholewa kutokana na Jean Baptiste Musabyimana, *Habari za Wakulima: Wakulima Amkeni* (2008)



https://xtremepape.rs/

**Matini C**

# Singida: Mkoa wa Madini Tanzania

❶ Si watu wengi wanauhusisha mkoa wa Singida na utajiri wa madini, lakini ukweli ni kwamba mgodi wa kwanza mkubwa wa dhahabu nchini ulijengwa mkoani Singida mwaka 1907. Kamishna msaidizi wa madini kanda ya kati, Sosthenes Massola ameliambia gazeti la *Raia Mwema* kuwa mkoa wa Singida una madini ya aina mbalimbali ambayo hayapatikani maeneo mengine nchini ambayo yamekuwa yakisafirishwa nje ya nchi. Anasema mgodi wa Sekenke ulikuwa wa kwanza katika mkoa wa Singida ambao ulianza kujengwa mwaka 1907 na kuanza uzalishaji mwaka 1909 ukiwa mgodi mkubwa wa dhahabu hapa nchini. Madini yanayopatikana katika mkoa wa Singida ni pamoja na dhahabu, shaba, almasi na madini ya vito.

❷ **Ugunduzi mpya**

Hivi karibuni, watafiti nchini Tanzania wamegundua kuweko kwa madini mengi aina ya almasi pamoja na dhahabu mkoani Singida. Madini haya yanapatikana katika mlima Kimbalati wilayani Iramba. Watafiti hawa wamekuwa wakitafiti kuhusu upatikanaji wa madini nchini. Kuwepo kwa madini kumeifanya kanda ya kati kushika nafasi ya pili kwa kuwa na madini mengi ikitanguliwa na kanda ya Ziwa. Mtendaji mkuu wa watafiti, Profesa Abdul Mruma ameliambia gazeti la *Raia Mwema* kuwa madini hayo yaligundulika baada ya upimaji kufanyika kwa kutumia ndege maalum za kupimia madini chini ya ardhi. "Tumezoea kuona almasi inapatikana Mwadui mkoani Shinyanga na maeneo ya Kahama, lakini sasa tumeweza kugundua madini ya almasi mengi mkoani Singida yanayopatikana katika mlima Kimbalati wilayani Iramba." Alisema.

❸ Mtafiti huyu anashauri kwamba, ili kuhakikisha wananchi wananufaika na kuwepo na madini katika maeneo yao, ni vyema serikali kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo ambao wataweza kuungana na wanabiashara wakubwa ili waweze kuwainua katika faida na wachimbaji wadogo wapate manufaa zaidi.

❹ Wataalam wamewaonya wananchi kuwa kuwepo kwa madini ya aina tofauti katika mkoa wa Singida huku mengine kama ya almasi yakiendelea kugunduliwa, yanaweza yasilete faida kwa wananchi husika iwapo serikali haitaweka utaratibu mzuri wa kuyachimba.

Matini imetoholewa kutokana na *Raia Mwema: Muungwana ni Vitendo*, www.raiamwema.co.tz (2016)

https://xtremepape.rs/

**Matini D**

# Punda Mjini Lamu

❶ Katika Mji wa Lamu, Punda huachiliwa huru na kuzunguka kila mahali. Hali hii husababisha mazingira kuchafuka. Wakazi wa Lamu na viongozi wao wamekasirishwa na uchafuzi huu wa mazingira. Gavana wa Lamu Bw. Issa Timamy amesema kwamba kutaundwa sheria ya kuadhibu watu wanaoachilia punda kuzurura mjini humo.

❷ Punda huchafua mazingira kwa kinyesi chao. Wafanyikazi wa kusafisha barabara wanafanya bidii kusafisha lakini kazi hii imekuwa ngumu. Sheria ya uhifadhi wa mazingira haya itapunguza ugumu wa kazi ya kusafisha mazingira.



❸ Sheria hiyo itahusu punda wanaozurura kukamatwa na kufungiwa kwenye vibanda. Punda hawa watakaa kwenye vibanda hadi mwenye punda atakapolipa faini. Faini itakuwa kati ya shilingi mia tano hadi elfu tatu. Faini itategemea idadi ya punda. Mwenye punda wengi atalipa pesa nyingi.

❹ Wakazi wa Lamu wameliambia gazeti la *Taifa Leo* kwamba wamefurahishwa sana na sheria mpya ya uhifadhi wa mazingira. Walisema kwamba sheria hii itasaidia kutunza usafi wa mazingira ya Lamu. Sheria hii pia itawafanya wakazi wa Lamu kuwalinda punda wao vizuri.

❺ Punda wanapoachiliwa huzurura maeneo mbalimbali mitaani. Kwa mfano, punda hawa huenda katika maeneo ya takataka wanapotafuta chakula. Wanapopata chakula hukibeba na kingine hukiangusha njiani na kuchafua mazingira haya. Hali hii huhatarisha afya ya wakazi wa mji huu.

❻ Kinyesi cha punda hufanya mazingira kuonekana mabaya. Pia, mazingira haya machafu huwa ni makao ya inzi ambao huzaliwa kwa wingi. Inzi hawa hueneza magonjwa mbalimbali ambayo huhatarisha maisha ya wakazi wa Lamu. Uchafu pia huharibu hewa kwa kutoa harufu mbaya.

❼ Mazingira machafu pia hayawapendezi watalii. Biashara ya utalii itaenda chini iwapo wenyeji hawatazingatia usafi. Lamu ni mmojawapo wa miji ambayo iko mstari wa mbele katika kuhifadhi utamaduni wa Waswahili. Ni muhimu kutunza usafi wa mji huu ili watalii wafurahie mazingira safi.

❽ Hata hivyo, punda wamewasaidia sana wakazi wa Lamu. Wamekuwa wakibeba watu, mitungi ya maji na mizigo ya aina mbalimbali. Hali hii imerahisisha usafiri mjini Lamu.

Matini imetoholewa kutokana na Kalume Kazungu, *Taifa Leo, Alhamisi* (2016)
(Picha: The Donkey Sanctuary)

https://xtremepape.rs/